MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.26. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Juni 11-20, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 21-30, 2023*

## MUHTASARI


- Maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa makavu na hali ya ubaridi kiasi.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia ukaushaji, uvunaji na utunzaji wa mazao.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii ilichangia kuongezeka kwa kasi ya upepo katika maeneo ya mwambao wa pwani. Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa na mchango kidogo katika kusafirisha hewa yenye unyevunyevu kuelekea katika ukanda wa pwani ya nchi. Joto la Bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki na mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) lilikuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Katika kipindi hiki maeneo mengi ya nchi yalikuwa makavu kwa ujumla. Kiasi cha juu cha mvua cha milimita 51.4 kimerekodiwa katika kituo cha Ukiriguru mkoani Mwanza na milimita 31.0 katika kituo cha Bukoba mkoani Kagera kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Juni 11-20, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Katika kipindi hicho cha dekadi, baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wakulima walikuwa wanajihusisha zaidi na uvunaji na uhifadhi wa mahindi na mpunga, isipokua kwa maeneo ya mikoa ya Mbeya na Njombe ambako zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa na kukauka. Kwa ujumla zao la mahindi na mpunga katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka liliendelea kuwa katika hali nzuri.

Kwa upande mwingine, zao la mahindi katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera, Morogoro, Arusha na Pwani limeripotiwa kuwa katika hatua ya kukomaa. Hali ya ukavu imesaidia ukuaji wa zao la mpunga lililoripotiwa kuathiriwa na maji yaliyotuama mashambani katika mkoa wa Pwani dikadi iliyopita.

Maji na malisho ya mifugo nchini kwa ujumla viliendelea kuwa katika hali nzuri.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vilikuwa katika hali ya kawaida katika maeneo mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2023

Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kidogo na ile iliyopo katika kizio cha kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuongeza kasi ya upepo katika maeneo ya mwambao wa pwani ya nchi. Joto la Bahari la wastani katika eneo la mashariki ya bahari ya Hindi na juu kidogo ya wastani katika eneo la magharibi mwa Bahari Hindi, linatarajiwa kuwa na mchango kidogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Kongo kuelekea Magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa makavu na yenye vipindi vifupi vya mvua nyepesi.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2023

Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika maeneno mengi ya nchi itasaidia katika kukomaa kwa mahindi pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mavuno zinazoendelea.

Mvua nyepesi zinazotarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa Ziwa Victoria na pwani ya kaskazini zinatarajiwa kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao hususan mahindi ambayo yapo katika hatua ya kukomaa.

Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao mashambani ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wafugaji pia wanashauriwa kuhakikisha mifugo yao inalindwa dhidi ya hali mbaya ya hewa na magonjwa.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi.

Jamii inashauriwa kuendelea kutumia maji yaliyopo kwa uangalifu kufuatia kuanza kwa msimu wa ukavu na baridi katika maeneo mengi nchini.